

Uchambuzi wa Mashartizuizi katika Muundo wa Silabi za Kichasu

Rabiel Fadhili¹ na Faraja Mwendamseke²

Ikisiri

Makala hii imechunguza muundo wa silabi za lugha ya Kichasu kwa kuzingatia uchambuzi wa mashartizuizi ya Kichasu. Lengo la makala hii ni kubainisha miundo ya silabi za lugha hiyo. Utuftuti wa udhihirikaji wa miundo ya silabi katika lugha mbalimbali za Kibantu ndio umechagiza kufanyika kwa utafiti huu. Kutokana na tafiti mbalimbali, kila lugha huwa na mpangilio tofauti wa mashartizuizi na ujitokezaji wa miundo yake huweka mipaka katika miundo ya silabi zake katika maneno. Data zilikusanywa kwa kutumia upitiaji maandiko pamoja na masimulizi kutoka kwa watoataarifa. Data zilichanganuliwa kwa mkabala wa kitaamuli ambapo mbinu ya uchanganuzi kimada imetumika. Uchanganuzi wa data uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Umbo Upeo (1993). Matokeo yanaonesha kwamba Kichasu kina jumla ya miundo kumi na mmoja ya silabi inayokubalika kisarufi. Miundo hiyo ni ya silabi nyepesi na ya silabi nzito.

1.0 Utangulizi

Kichasu ni lugha inayozungumzwa kwa kiasi kikubwa katika eneo la wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro ikilinganishwa na maeneo mengine (LOT, 2009). Lugha hii ina lahaja kuu mbili ambazo zimetokana na utengano asilia wa kijiografia, Kichasu cha Kaskazini na Kichasu cha Kusini (Nurse na Philippson, 2003; Maho, 2009). Nurse na Philippson (2003) na Maho (2009) wanaibainisha lugha ya Kichasu katika kanda G20 katika kundi la Kishambala. Katika ubainishaji wao, Kichasu kimewekwa katika kundi dogo la G22 na kugawanywa katika makundi mengine mawili madogo ya Kichasu cha Kaskazini ambacho kimewekwa katika kundi la G22A na Kichasu cha Kusini ambacho kimewekwa katika kundi la G22B. Aidha, lahaja ya Kichasu cha Kusini inaoneshwa kuwa na aina kadhaa za vilahaja ambavyo ni Kisuji/Kimamba (Kotz, 1909), Kimbaga na Kigonja (Kagaya, 1989; Mreta, 1998) na Kimakasa-papa (Omari, 1991; Mreta, 1998). Kuwapo kwa vilahaja hivyo kumetokana na utengano wa kijiografia baina ya Wachasu wa Kusini uliokuwapo kwa miaka mingi tangu kipindi cha kuhamahama (Yohana,

¹ Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe:
rabielfadhili@gmail.com

² Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe:
fmwendamseke@gmail.com

2009; Juma, 2018). Utafiti huu umehusisha wazungumzaji wa kilahaja cha Kimakasa-papa kama sehemu ya lahaja ya Kichasu cha Kusini kinachozungumzwa katika kata ya Hedaru na Mabilioni kwa sababu ni lahaja ambayo haijaandikiwa sana ikilinganishwa na lahaja ya Kichasu cha Kaskazini.

Aidha, katika kipengele tafiti mbalimbali zilizokwishakufanyika katika lugha ya Kichasu, imebainika kuwa hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanyika katika lugha ya Kichasu kuhusiana na miundo ya silabi zake. Wanaisimu wamekuwa wakikibainisha Kichasu kuwa ni mionganoni mwa lugha zenyenye muundo wa silabi huru bila kutoa ufanuzi wa kina na kuibainisha miundo husika (taz. Kagaya, 1989; Mreta 1998; Mreta, 2008). Kwa hiyo, kutobainishwa kwa miundo ya silabi katika Kichasu ndiko kuliibua ari ya utafiti huu kufanyika ili kuchunguza miundo ya silabi za lahaja hii.

Silabi ni kipengele muhimu sana katika fonolojia ya lugha iwayo yoyote (Fery na Vijver, 2003; Hyman, 2003; Nkamigbo, 2015). Fery na Vijver (2003) wanatilia mkazo hoja ya umuhimu wa silabi katika lugha wanapoeleza kwamba ili mtu aweze kujua lugha ni lazima aijue fonolojia ya lugha husika. Aidha, kujua fonolojia ya lugha fulani ni hatua muhimu ya awali katika kuielewa misingi ya lugha hiyo. Vilevile, Kenstowicz (1994) anaweka bayana kuwa kila lugha inahitaji kufanyiwa tafiti ili kufanya majumuisho ambayo yanaweza kuthibitishwa. Kwa hiyo, kufanya utafiti wa miundo ya silabi za Kichasu ni sawa na kuieleza fonolojia ya lugha hiyo. Hii inatokana na kuwa silabi ndiyo misingi wa fonolojia ya lugha (taz. Abercrombie, 1967; Hyman, 1985; Nkamigbo, 2015).

Tafiti nyingi zimechunguza muundo wa silabi katika lugha za Kibantu (mathalani, taz. Hyman na Katamba, 1999; Odden na Odden, 1999; Kimizi, 2003; Kigume, 2010; Charles, 2011; Massamba, 2011; Choti, 2015; Odden, 2015; Persohn, 2017; Downing na Mtenje, 2017; Etakwa, 2019). Katika tafiti hizo, jambo linalojidhihirisha ni kwamba silabi kama kipengele muhimu cha kifonolojia ni changamani. Kipengele hicho hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine kwa sababu kila lugha ina mashartizuizi yake ambayo hutawala muundo wa silabi zake (taz. Abercrombie, 1967; Clark na Yallop, 1990; Ladefoged, 2000; Odden, 2006). Kila lugha ina mashartizuizi mahususi yanayoweka mipaka katika muundo wa silabi zake katika maneno. Mashartizuizi hayo ndiyo yanayoelekeza sauti fulani iandamane na aina gani ya sauti na si vinginevyo. Hatimaye, hudhihirisha muundo wa silabi katika lugha husika ulio na upekee. Rejelea mfano Na. (1) wa miundo ya silabi kutoka katika lugha tatu za Kibantu.

- | | | |
|-----|---------------------------------------|------------|
| (1) | a. ywa
\$ywa\$
'ngumu sana' | [Kisukuma] |
| | b. mukane
\$m\$ka\$ne\$
'kataa' | [Kingindo] |

c. sinkhaala	[Kichewa]
\$si\$n\$kha:\$la\$	
‘sitakaa’	

Chanzo: Kindija (2003); Kigume (2010); Downing na Mtenje (2017)

Katika mfano Na. (1) a-c, inabainika kuwa kuna miundo tofautitofauti ya silabi kutokana na mashartizuizi yaliyopo katika kila lugha. Katika mifano hiyo, kuna silabi zenyenye muundo wenye mfuatano wa viyeyusho viwili na irabu (YYI) kama unavyojitokeza katika lugha ya Kisukuma. Pia, kuna muundo wenye konsonanti na irabu (KI) na muundo wa nazali peke yake (N) kama inavyojitokeza katika lugha ya Kingindo na Kichewa.

Akifafanua kuhusiana na lugha za Kibantu, Massamba (2011) anaweka wazi kwamba muundo wa silabi katika lugha za Kibantu hutofautiana kwani kila lugha ina mashartizuizi yake ya usilabishaji. Kulingana na Katamba (1989), lugha zina kanuni tofautitofauti za usilabishaji. Hivyo, tofauti baina ya lugha hutegemea upekee wa kanuni za lugha husika. Clements na Keyser (1983) na Choti (2015) wanabainisha kuwa muundo msingi wa silabi katika lugha za Kibantu ni ule wa konsonanti na irabu (KI) na kwamba miundo mingine inategemea mashartizuizi ya lugha husika. Mathalani, Odden na Odden (1999) wanasema muundo wa silabi za lugha ya Kihehe umegawanyika katika aina kumi. Aina hizo ni irabu pekee (I), irabu ndefu pekee (I:), konsonanti na irabu (KI), konsonanti na irabu ndefu (KI:), nazali, konsonanti na irabu (NKI), nazali, konsonanti na irabu ndefu (NKI:), konsonanti, kiyeyusho na irabu (KYI), konsonanti, kiyeyusho na irabu ndefu (KYI:), nazali, konsonanti, kiyeyusho na irabu (NKYI) na nazali, konsonanti, kiyeyusho na irabu ndefu (NKYI:). Aidha, katika muundo wa I:, KI:, NKI:, KYI: na NKYI:, mfuatano wa irabu mbili hutokana na mchakato wa uyeyushaji. Mfano Na. (2) katika Kihehe unathibitisha hilo.

(2) lyeendwa	\$li:\$e\$ndwa\$	‘tapendwa’
lyeeheela	\$li:\$e\$he:\$la\$	‘tapumua’
kwoogopa	\$ku:\$o\$go\$pa\$	‘kuogopa’
kwuusa	\$ku:\$u\$sa\$	‘kuja’

Chanzo: Odden na Odden (1999)

Mfano Na. 2 unadhihirisha kwamba lugha ya Kihehe hairuhusu mfuatano wa /j/ kabla ya /e/ na /w/ kabla ya /o/, /u/; hivyo, kufanya kuwa na muundo wa silabi wenye irabu zilizorefushwa. Aidha, mchakato huo pia unajibainisha katika Luganda (Hyman na Katamba, 1999) na Kimatumbi (Odden, 1996). Odden (2015) anaeleza kuwa katika lugha nyingi za Kibantu irabu inayofuata katika muundo wa silabi wenye mfuatano wa nazali na konsonanti (NK) huwa inarefushwa, kama ilivyo katika Kihehe ambapo kurefushwa huko kunatokana na mchakato wa kifonolojia.

Downing na Mtenje (2017) waliifafanua fonolojia ya lugha ya Kichewa ambapo, pamoja na mambo mengine, walibainisha muundo wa silabi. Wanaeleza kuwa muundo msingi wa silabi katika lugha ya Kichewa ni ule unaoundwa na konsonanti na irabu na kwamba muundo huo huweza kujibainisha pande zote za neno. Aidha, wanaeleza kuwa ni lazima maneno yote yaishie na irabu. Miundo mingine inategemea mashartizuizi ya lugha hiyo. Mfano Na. (3) unadhihirisha miundo hiyo.

(3) mwaa-na	\$mwa:\$na\$	'mtoto'
ii-dya	\$i:\$dya\$	'kula'
dyoola	\$dyo:\$la\$	'safisha'
cii-ndwi	\$ci:\$ndwi\$	'hamasa'

Chanzo: Downing na Mtenje (2017)

Mfano Na. 3 unaonesha miundo ya silabi tofautitofauti kulingana na mashartizuizi ya lugha ya Kichewa. Kuna muundo wa silabi wenye mfuatano wa konsonanti halisi na viyeyusho unaokubalika, ambapo kiyeyusho /w/ hakina mipaka ya utokezaji yaani kinaweza kutokea kabla ya mzizi au mwanzoni au mwishoni mwa mzizi. Tofauti na ilivyo kwa kiyeyusho /j/ ambacho hujibainisha mwanzoni mwa mzizi wa neno. Halikadhalika, muundo wenye nazali, konsonanti na kiyeyusho nao unakubalika katika Kichewa.

Baadhi ya lugha huruhusu uwanja mpana wa aina ya silabi zikitawaliwa na mashartizuizi mengi katika uundaji wa miundo yake na michakato inayoathiri miundo husika. Vilevile, idadi ya miundo ya silabi ni tofauti baina ya lugha moja hadi nyingine (taz. Kimizi, 2003; Kigume, 2010; Charles, 2011; Zacharia, 2013; Judica, 2014). Hivyo, tafiti hizo zimeamsha ari ya utafiti huu kufanyika ili kuweza kubaini muundo wa silabi za Kichasu kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha hiyo. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, sehemu ya pili inahusu methodolojia ya utafiti na misingi ya nadharia, sehemu ya tatu inahusu muundo wa silabi katika lugha ya Kichasu na sehemu ya nne ni hitimisho.

2.0 Methodolojia ya Utafiti na Misingi ya Nadharia

Ili kufikia lengo kuu la utafiti huu ambalo ni kuchunguza muundo wa silabi katika lugha ya Kichasu, utafiti huu umehusisha vyanzo viwili vya data: maktabani na uwandani. Vyanzo hivi vilitumika kupata data ya upili na data ya msingi mtawalia. Kwa upande wa maktabani, data zimepatikana kutoka katika matini mbalimbali za kisarufi. Machapisho ya kisarufi yaliyotumika ni pamoja na chapisho la Kagaya (1989), ambalo linahusu sarufi ya Kichasu pamoja na *Kamusi ya Kichasu-Kiingereza-Kiswahili* (Mreta 2008). Sampuli ya matini hizo ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Kwa mujibu wa Vaux na Cooper (2003), sampuli lengwa inapatikana kwa kuchagua vyanzo vya taarifa ambavyo vina sifa za kipekee zinazofaa kulingana na malengo ya utafiti husika. Hivyo, ili kupata data

halisi za muundo wa silabi katika Kichasu, utafiti huu uliteua matini ambazo zinahusu lugha ya Kichasu ambamo ndani yake kuna orodha ya maneno yanayoonesha muundo wa silabi za Kichasu. Kutoka katika matini hizi, data zilikusanywa kwa mbinu ya upitiaji maandiko maktabani. Vyanzo hivi vilitoa data muhimu kuhusu silabi zilizopo katika lugha ya Kichasu ambapo muundo wake ulichanganuliwa kwa kuzingatia mashartizuizi yaliyopo katika lugha hii.

Aidha, data za uwandani zilikusanywa katika mazingira halisi ili kuongezea data zilizopatikana maktabani. Data za uwandani zilikusanywa kutoka katika vijiji vya Hedaru na Mabilioni vilivyopo katika kata za Hedaru na Mabilioni mtawalia, wilayani Same katika mkoa wa Kilimanjaro. Wilaya hii iliteuliwa kwa mbinu ya usampulishaji lengwa kwa sababu kwa mujibu wa LOT (2009) katika maeneo haya ndiko wanapatikana wazungumzaji wengi wa Kichasu cha Kusini. Katika mbinu ya usampulishaji lengwa, lengo lilikuwa kuwapata wazungumzaji wa lugha ya Kichasu. Aidha, kata na vijiji viliviyotumika viliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi. Mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ilitumika ili kuzipata kata mbili na vijiji viwili kutoka kundi kubwa. Hivyo, katika mbinu hii kata zote na vijiji vyote kwa kila kata viliorodheshwa, kisha kata na vijiji vilichaguliwa kutoka makundi hayo bila kufuata utaratibu maalumu. Hivyo, kata na vijiji viliviyoteuliwa vilitumika tu kama viwakilishi vya maeneo hayo yanayozungumzwa Kichasu. Watoataarifa 6 katika maeneo haya waliteuliwa kwa kuzingatia mgawanyo sawia wa kata zilizoteuliwa. Kwa hiyo, waliteuliwa watoataarifa 3 katika kila kata. Sampuli hiyo iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji tajwa. Vaux na Cooper (2003) wanafafanua kuwa katika mbinu hii mtafiti anaweza kuwatumia viongozi wa eneo lililoteuliwa kuweza kupata watoataarifa wachache watakaoweza kuwataja wenzao kulingana na vigezo ambavyo mtafiti atavibainisha. Hivyo, kwa kutumia mbinu hiyo, tuliwatumia viongozi wa vijiji tulivyoviteua kututajia mtoataarifa mmoja anayezungumza Kichasu. Baada ya hapo katika kila kijiji kila mtoataarifa mmoja aliyetajwa aliombwa ataje watoataarifa wawili wanaozungumza Kichasu. Kwa hiyo, wakafikia watoataarifa 6 ambapo idadi hii ilikuwa faafu kwa sababu iliweza kutosheleza mahitaji ya data za utafiti huu.

Katika kukusanya data uwandani, mbinu ya kukusanya masimulizi ya hadithi ilitumika. Mbinu hii ilitumika kwa sababu hadithi huwa na maneno mengi zaidi tofauti na kutaja tu maneno, virai na vishazi pwekepweke. Hivyo, kila mtoataarifa mmoja aliombwa asimulie hadithi moja ambapo hadithi sita (6) kutoka kwa washiriki sita (6) zilikusanywa. Hadithi hizi zilihusu mada mbalimbali, kama vile matukio ya asili, historia na utamaduni. Hivyo, masimulizi yalisikilizwa na kurekodiwa ili kubaini jinsi lugha ya Kichasu inavyozungumzwa. Hivyo, mbinu hii ilitumika kupata data za kutosha za maneno yenye kuonesha aina za miundo ya silabi za Kichasu. Kwa hiyo, silabi zilibainishwa na namna miundo yake inavyojitokeza kutoka katika masimulizi hayo. Kwa kutumia njia hizi za utafiti,

mtafiti alipata data kuhusu silabi katika lugha ya Kichasu kwa kuzingatia muundo wake ili kutimiza malengo ya utafiti.

Sambamba na hayo, mkabala wa kitaamuli ulitumika katika uchanganuzi wa data. Katika mkabala wa kitaamuli, mbinu ya uchanganuzi kimada ilitumika ambayo huzingatia kuhusisha mawazo ya jambo linalotafitiwa kwa kutazama jinsi linavyojitokeza katika data zilizokusanywa, ambalo katika utafiti huu ni miundo ya silabi. Aidha, katika ufanuzi wa data, tumetumia majedwali kuonesha kwa uwazi namna mashartizuizi yanavyofanya kazi katika kupata miundo sahihi ya silabi za Kichasu.

Utafiti huu uliongozwa na mawazo ya Nadharia ya Umbo Upeo. Nadharia hii iliasisiwa na Allan Prince pamoja na Paul Smolensky mnamo mwaka 1993 (Kager, 2004). Madai ya msingi ya Nadharia ya Umbo Upeo yamekitwa katika msingi kwamba miundo ya lugha mbalimbali hutokana na ukinzano kati ya mashartizuizi ya kimajumui yaliyopo na kwamba tofauti zilizopo kati ya lugha za binadamu hutokana na tofauti za thamani ya mashartizuizi yanayohusu mpangilio ama wa sauti, maneno au virai. Kager (*keshatajwa*) anaeleza kwamba mashartizuizi ni masharti yanayotoa mwongozo wa namna ya kupata umbo fulani kwa usahihi na hubainisha yanayopaswa kufanyika na yasiyopaswa kufanyika katika sarufi za lugha.

Nadharia ya Umbo Upeo imekitwa katika misingi mikuu mitatu ambayo ni: zalishi, mashartizuizi na tathmini. Zalishi ni kijenzi kinachohusika na uzalishaji wa maumbotokeo katika lugha ambayo ndiyo yanashindanishwa ili kupata umbo lililofikia upeo wa ukubalifu. Mashartizuizi ni kijenzi ambacho kinahusika na uwekaji wa vigezo na masharti yanayoweza kuvunjwa na yasiyoweza kuvunjwa. Vigezo hivyo ndivyo huamua umbo lipi katika maumboshindani limefikia upeo wa ukubalifu. Tathmini kwa upande wake ni kijenzi katika Nadharia ya Umbo Upeo ambacho kinahusika na kuamua umbo lipi katika maumbotokeo limefikia upeo wa ukubalifu na kushinda. Tathmini huangalia kati ya washindani ni mshindani yupi amevunja mashartizuizi machache yanayovumilika na yale yasiyovumilika. Misingi hii inafanya kazi pamoja na mihimili yake ambayo ni: umajumui, ukiukwaji, upangiliaji na usambamba.

Nadharia hii imetumika kwa kuyapangilia mashartizuizi ya muundo wa silabi za Kichasu ili kuona ukiukwaji au ufuatwaji wake kwa kufanya tathmini ya umbo lipi katika maumbo yote lililofikia upeo wa ukubalifu. Upangiliaji huo umeongoza upataji wa muundo sahihi wa silabi kwa msingi kwamba muundo wa silabi ni matokeo ya mwingiliano wa mashartizuizi ya uadilifu na uziada. Mashartizuizi ya uadilifu huzingatia mfanano kati ya umbotokeo na umboghaflinaloingizwa. Mashartizuizi ya uziada huruhusu mabadiliko baina ya umboghaflina umbotokeo katika kupata muundo wa silabi uliofikia upeo wa ukubalifu. Kwa minajili hiyo, Nadharia ya Umbo Upeo imefaa katika uchanganuzi wa data za utafiti huu.

3.0 Muundo wa Silabi za Lugha ya Kichasu

Uainishaji wa muundo wa silabi za Kichasu ulizingatia uzito wa silabi ambapo dhana ya uzito wa silabi huzingatia aina ya irabu inayounda muundo fulani wa silabi. Hivyo, uainishaji huu ulizingatia miundo ya silabi zenyne irabu zisizo na wakaa katika utamkaji, yaani silabi nyepesi na irabu zenyne wakaa katika utamkaji, yaani silabi nzito. Kwa msingi huo, miundo ya silabi za lugha ya Kichasu imechanganuliwa kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha ya Kichasu. Mashartizuizi yaliyotumika ni: kila muundo wa silabi lazima uwe na kilele, yaani kuwa na irabu (KILELE); umbo lifikie ukomo wa ukubalifu, yaani kusiwe na udondoshaji wa vitamkwa (FIKI-UKO); umbo litegemee uasili wake, yaani kusiwe na uchopekaji wa vitamkwa (TEGE); umbo lishabihiane katika matamshi (SHABI); umbo lisiihie na koda, yaani konsonanti (H-KODA); umbo lenye nazali /n/ na /m/ inapokuwa imeanza sambamba na irabu /i/ na /u/ hairuhuswi kufuatiwa na konsonanti halisi ($*N_{(n+m)} > I_{(i+u)} + K$); umbo ambalo konsonanti ya kwanza lazima iwe nazali halafu ifuatiwe na konsonanti halisi (N>K); umbo ambalo konsonanti ya kwanza lazima iwe nazali halafu ifuatiwe na kiyeyusho ambacho chawenza kuwa /y/ ama /w/ (N>Y); umbo ambalo kunakuwa na mfuatano wa konsonanti, kiyeyusho na irabu (KYI); umbo ambalo lina mfuatano wa irabu ndefu katika silabi (I:). Aidha, vifupisho vilivyopo katika mabano ndivyo vilivyotumika katika majedwali kuonesha mashartizuizi husika. Hivyo, uchambuzi wa muundo wa silabi za Kichasu kwa kuzingatia mashartizuizi hayo umewasilishwa katika vipengele vinavyofuata.

3.1 Muundo wa Silabi Nyepesi katika Kichasu

Kama tulivyofafanua dhana ya silabi nyepesi na nzito katika kipengele cha 3.0, miundo ya silabi nyepesi katika Kichasu inawasilishwa katika vipengele vinavyofuata.

3.1.1 Muundo wa Irabu (I)

Kulingana na data za utafiti, aina hii ya muundo wa silabi katika lugha ya Kichasu huweza kujitokeza mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno kama Data Na. (1) inavyobainisha.

(1) igana	\$i\$ga\$na\$	‘mia’
iyavo	\$i\$a\$vo\$	‘kesho’
iguo	\$i\$gu\$o\$	‘jana’
etongie	\$e\$to\$ngi\$e\$	‘alienda’

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Kama Data Na. (1) inavyoonekana, kwenye data zenyne hati iliyokoza, huu ni muundo pekee wa Kichasu usiokuwa na mwanzosilabi. Katika upangiliaji wa mashartizuizi ya Kichasu, shartizuizi lenye nguvu katika aina hii ya muundo ni KILELE linalohitaji muundo wa silabi kuwa na irabu. Mfano katika Jedwali Na. 1 unaonesha mashartizuizi kama yalivyo kimpangilio na namna tathmini

iliyofanyika katika ukiukwaji na ufuatwaji wake katika kupata muundo wa aina hii wa silabi za Kichasu uliofikia upeo wa ukubalifu.

Jedwali Na. 1: Muundo wa Silabi wa Irabu (I)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI			
		KILELE	FIKI-UKO	TEGE	SHABI
igana	a. \$ ³ iga\$na\$			** ⁴	* ⁵
	b. \$ig\$a\$na\$	**! ⁶	**	**	*
	c. \$i\$ga\$na\$				

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Katika Jedwali Na. 1, uchanganuzi unaonesha umboshindani (a) limekiuka shartizuizi la tatu na la mwisho kimpangilio. Aidha, umboshindani (b) limekiuka shartizuizi la msingi na lenye nguvu, la pili, la tatu na la mwisho kimpangilio. Umboshindani (c) halikuvunja shartizuizi lolote na hivyo kuwa mshindi mionganini mwa maumboshindani mengine ambayo ni umbo (a) na (b).

3.1.2 Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI)

Aina hii ya muundo hujumuisha konsonanti moja na irabu moja, na hivyo kuwa ni muundo wenye mwanzosilabi. Hivyo, Kichasu kinaruhusu muundo mama wa silabi za Kibantu. Kimsingi, ujibainishaji wa aina hii ya muundo katika Kichasu ni mkubwa sana kwa sababu mwanzosilabi huweza kuundwa na sauti yoyote ya konsonanti. Aina hii ya muundo huweza kujibainisha mwanzoni, kati na mwishoni mwa neno kama Data Na. (2) inavyodhahirisha.

(2)	hale	\$ha\$le\$	‘mbali’
	uvivi	\$u\$vi\$vi\$	‘ubaya’
	tebanda	\$te\$ba\$nda\$	‘hanenepi’
	vala	\$va\$la\$	‘wale’

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Muundo huu wa silabi katika lugha ya Kichasu, kwenye Data Na. (2), hususani zile zenye chapa iliyokoza, unaonesha kwamba konsonanti zisizo na usilabi hufuatiwa na irabu. Hii inaonesha kuwa sauti za konsonanti zinazounda aina hii ya muundo ni zile zisizo na sifa ya usilabi. Aina hii ya muundo huamuliwa na shartizuizi lenye nguvu katika Kichasu linalohitaji silabi kutoishia na konsonanti, yaani H-KODA. Mpangilio wa mashartizuizi kimfuatano katika kubaini muundo wa silabi uliofikia upeo wa ukubalifu kulingana na sarufi ya lugha ya Kichasu unaoneshwa katika Jedwali Na. 2.

³ Alama hii imetumika kuonesha mpaka wa silabi.

⁴ Alama hii imetumika kuonesha uvunjifu wa shartizuizi la kawaida lisilovumilika.

⁵ Alama hii imetumika kuonesha uvunjifu wa shartizuizi linalovumilika.

⁶ Alama hii imetumika kuonesha uvunjifu wa shartizuizi la nguvu lisilovumilika.

Jedwali Na. 2: Muundo wa Silabi wa Konsonanti na Irabu (KI)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		H-KODA	FIKI-UKO	SHABI
vala	a. \$va\$la\$			
	b. \$val\$a\$	**!	**	*
	c. \$v\$al\$a\$	**!	**	*

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Katika Jedwali Na. 2, tunabaini kuwa umboshindani (a) ndilo lililoshinda kwa kuwa halijakiuka shartizuizi lolote. Aidha, umboshindani (b) limevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Vilevile, umboshindani (c) limevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio, hivyo, kufanya kushindwa kuwa mshindi. Maumboshindani (b) na (c) yamekiuka mashartizuizi yenye nguvu katika Kichasu na hivyo hayakubaliki katika miundo ya silabi za Kichasu.

3.1.3 Muundo wa Nazali (N)

Hii ni aina nyingine ya muundo wa silabi za lugha ya Kichasu ambapo ujitokezaji wake husababishwa na udondoshaji wa irabu /u/ na /i/ hasa zinapotangamana na nazali /m/ na /n/ na zinapofuatiwa na konsonanti halisi. Vilevile, muundo huu wa silabi hujibainisha mwanzoni na katikati mwa neno kama inavyodhihirishwa na Data Na. (3).

(2)	msavi	\$m\$sa\$vi\$	‘mchawi’
	mshukule	\$m\$shu\$ku\$le\$	‘msukule’
	amtongie	\$a\$m\$to\$ngi\$e\$	‘amwendee’
	ntangwa	\$n\$ta\$ngwa\$	‘ninaitwa’

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Tukichunguza Data Na. (3), hususani zile zenye hati iliyokoza, tunaona kwamba katika aina hii ya muundo shartizuizi lenye nguvu na linalotawala mashartizuizi mengine yote ni lile linaloweka mipaka ya irabu /i/ na /u/ kutotokea kati ya nazali na konsonanti halisi ($*N_{(n+m)} > I_{(i+u)} + K$). Hivyo, Jedwali Na. 3, limeonesha kwa muhtasari upangiliwaji wa mashartizuizi ili kuweza kuyafanya tathmini na kupata muundo wa silabi uliofikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu.

Jedwali Na. 3: Muundo wa Silabi wa Nazali (N)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		$*N_{(n+m)} > I_{(i+u)} + K$	TEGE	SHABI
msavi	a. \$m\$sa\$vi\$			

	b. \$ms\$a\$vi\$	**!	**	*
	c. \$msa\$v\$i\$	**!	**	*

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Data katika Jedwali Na. 3, kwenye zile zenyet hati iliyokoza, inadhihirisha kuwa umboshindani (a) ndilo mshindi dhidi ya maumbo mengine yaliyoshindanishwa kwani halijavunja shartizuizi lolote katika Kichasu. Maumbo yote (b) na (c) yamevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Hivyo, maumboshindani hayo hayakufikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu.

3.1.4 Muundo wa Nazali, Konsonanti na Irabu (NKI)

Kulingana na data za utafiti zilizokusanya, Kichasu ni lugha inayoruhusu pia mfuatano wa nazali, konsonanti na irabu katika miundo ya silabi zake. Aidha, utokeaji wake huweza kuwa mwanzoni, kati au mwishoni mwa neno na hivyo kutokuwa na kizuizi cha ujitekezaji. Jambo hili linabainishwa kwa uwazi katika Data Na. (4).

(4) nkcombe	\$nko\$mbe\$	‘kucha’
mramba	\$m\$ra\$mba\$	‘mbuyu’
ngombo	\$ngo\$mbo\$	‘fito’
mpembe	\$mpe\$mbe\$	‘pembe’

Chanzo: Kagaya (1989) na Mreta (2008)

Tukichunguza Data Na. (4), kwenye zile zenyet hati iliyokoza, tunabaini kuwa aina hii ya muundo hulazimu konsonanti ya kwanza kuwa nazali. Aidha, data hiyo inaonesha kwamba, katika Kichasu ni lazima konsonanti ya kwanza iwiane mahala pa matamshi na konsonanti inayofuata. Vilevile, data inaonesha kwamba katika Kichasu vipasuo mara zote ndivyo hufuatia baada ya nazali. Kwa msingi huo, shartizuizi linalotawala na lenye nguvu katika Kichasu ni lile linalotaka konsonanti ya kwanza kuwa nazali ikifuaatiwa na konsonanti halisi, yaani N>K. Jedwali Na. (4) linaonesha upangiliaji wa mashartizuizi katika aina hii ya muundo wa silabi ili kupata muundo wa silabi uliofikia upeo wa ukubalifu.

Jedwali Na. 4: Muundo wa Silabi wa Nazali, Konsonanti na Irabu (NKI)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		N>K	FIKI-UKO	SHABI
mramba	a. \$m\$ra\$mba\$			
	b. \$m\$ra\$mba\$a\$		**	**
	c. \$m\$ram\$ba\$	**!	**	**

Chanzo: Mreta (2008)

Tukichunguza Jedwali Na. 4, tunaona kwamba umboshindani (a) limeibuka mshindi dhidi ya maumboshindani mengine kwa kuwa halijavunja shartizuizi

lolote. Umboshindani (b) limevunja shartizuizi la pili na la mwisho kimpangilio. Kwa upande wa umboshindani (c), lenyewe limevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Hivyo, maumboshindani hayo hayakufikia upeo wa ukubalifu.

3.1.5 Muundo wa Nazali, Kiyeyusho na Irabu (NYI)

Data ya utafiti huu inaonesha kuwa lugha ya Kichasu inaruhusu mfuatano wa nazali, kiyeyusho na irabu katika silabi zake. Sehemu ya irabu huweza kujazwa na irabu yoyote isipokuwa /u/ ikiwa nazali imefuatiwa na /w/. Data Na. (5) huonesha utokeaji wa aina hii ya muundo.

(5)	mwire	\$mwi\$re\$	‘mwambie’
	mwiri	\$mwi\$ri\$	‘mwili’
	nyiru	\$nyi\$ru\$	‘nyeusi’
	hamwe	\$ha\$mwe\$	‘pamoja’

Chanzo: Mreta (2008)

Muundo wa silabi ulio katika Data Na. (5), kwenye zile zenye wino uliokoza, utokeaji wake si matokeo ya mchakato wowote wa kifonolojia bali ni matokeo ya sheria asilia za kifonetiki katika baadhi ya miundo kama vile \$ha\$mwe\$. Pia, baada ya kuchanganua data nzima tumegundua kuwa miundo mingine ni matokeo ya michakato ya kifonolojia, mathalani, \$mwi\$re\$ kama inavyojibainisha katika Data Na. 5 hapo juu. Katika miundo kama hii, mchakato wa uyeyushaji unaonekana kufanya kazi. Ni wazi kuwa konsonanti halisi ndiyo hutangulia na kufuatiwa na kiyeyusho pamoja na irabu.

Kadhalika, katika aina hii ya muundo shartizuizi linalotawala ni lile linaloelekeza kwamba, katika mfuatano wa konsonanti mbili, konsonanti ya kwanza lazima iwe nazali ikifuatiwa na kiyeyusho, yaani N>Y. Kupitia Jedwali Na. 5, mashartizuizi yanabainishwa kimpangilio katika kujaribu kubaini ukiukwaji au ufuatwaji wake ili kupata muundo wa silabi uliofikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu.

Jedwali Na. 5: Muundo wa Silabi wa Nazali, Kiyeyusho na Irabu (NYI)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		N>Y	H-KODA	FIKI-UKO
hamwe	a. \$ha\$mwe\$			
	b. \$ha\$mw\$e\$		**	**
	c. \$ham\$we\$	**!		**

Chanzo: Mreta (2008)

Katika Jedwali Na. 5, na kama tulivyoyapangilia na baada ya kufanya tathmini katika kubaini umboshindani lililofikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu,

tumebaini kwamba umboshindani (a) limefikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa halikuvunja shartizuizi lolote. Aidha, umboshindani (b) halikufikia upeo wa ukubalifu kwa sababu limevunja shartizuizi la pili na la mwisho kimpangilio. Halikadhalika, umboshindani (c) halikuweza kufikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa limevunja shartizuizi lenye nguvu na la mwisho kimpangilio.

3.1.6 Muundo wa Konsonanti, Kiyeyusho, na Irabu (KYI)

Silabi za Kichasu pia, kulingana na data zilizokusanya, zinaruhusu mfuatano wa konsonanti, kiyeyusho na irabu. Udhihirikaji wake huweza kuwa mwanzoni, kati na mwishoni mwa neno. Data Na. (6) hapa chini inabainisha muundo huu.

(6)	kivyere vwedi lukwi	\$ki\$ vye \$re \$vwe\$di\$ \$lu\$kwi\$	‘mkwe’ ‘wema’ ‘ukuni’
-----	---------------------------	--	-----------------------------

Chanzo: Kagaya (1989) na Mreta (2008)

Kama Data Na. (6) inavyoonekana, hususani zile zenye hati iliyokoza, baada ya uchanganuzi wa data nzima, imebainika kuwa maumbo yanayojidhihirisha ni kwamba mfuatano wa konsonanti wenyе /j/ katika Kichasu hujibainisha zaidi katika sehemu ya mzizi wa neno, hasa mwanzoni. Vilevile, baada ya uchanganuzi wa data tulizozikusanya kutoka kwa watoataarifa, tumegundua kuwa mfuatano wa konsonanti wenyе /w/ hauchagui konsonanti tangulizi, jambo ambalo ni tofauti katika /y/, ambapo tunaona kuwa ni baadhi tu ya konsonanti zinazoweza kuandamana na kiyeyusho hicho, hususani sauti za vikwamizi. Katika aina hii ya muundo, shartizuizi linalotawala ni lile linaloruhusu mfuatano wa konsonanti halisi, kiyeyusho na irabu, yaani KYI. Sanjari na hilo, mashartizuizi yanayotawala aina hiyo ya muundo katika Kichasu yameainishwa na kupangiliwa katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6: Muundo wa Silabi wa Konsonanti, Kiyeyusho na Irabu (KYI)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		KYI	H-KODA	FIKI-UKO
lukwi	a. \$lu\$kwi\$	**!	**	**
	b. \$lu\$kwi\$	**!		**
	c. \$lu\$kwi\$			

Chanzo: Mreta (2008)

Kama Jedwali Na. 6 linavyoonekana, tunabaini kwamba umboshindani (a) limekiuka shartizuizi lenye nguvu, la pili na la tatu. Kadhalika, umboshindani (b) limevunja shartizuizi lenye nguvu na la mwisho kimpangilio. Hivyo, maumbo hayo yanakosa sifa ya muundo uliofikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu. Hata

hivyo, umboshindani (c) halijavunja mashartizuizi yoyote, kwa hiyo, lina sifa ya ukubalifu katika Kichasu.

3.1.7 Muundo wa Nazali, Konsonanti, Kiyeyusho na Irabu (NKYI)

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa lugha ya Kichasu inaruhusu mfuatano wa nazali, konsonanti halisi, kiyeyusho na irabu. Aidha, konsonanti ya kwanza kabisa ni lazima iwe nazali /n/ ikiwa imejitokeza mwanzoni mwa neno, na /m/ ikiwa imejitokeza katikati ya neno. Sanjari na hilo, katika aina hii ya muundo, neno zima linaweza kuwa muundo kamili na katika maneno mengine hujitokeza mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. Aina hii haitokani na mchakato wowote wa kifonolojia kama Data Na. (7) inavyoonekana.

(7)	nkwavi	\$nkwa\$vi\$	‘mmasai’
	nkwi	\$nkwi\$	‘kuni’
	vambwie	\$va\$mbwi\$e\$	‘marafiki’
	nkware	\$nkwa\$re\$	‘kwale’

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Kama Data Na. (7) inavyoonekana, kwenye zile zenye hati iliyokoza, aina hii ya muundo inaongozwa na kutawaliwa na shartizuizi kuu linalohitaji kuwe na mfuatano wa nazali, konsonanti halisi, kiyeyusho na irabu, yaani NKYI katika lugha ya Kichasu. Upangiliaji wa mashartizuizi kimpangilio katika kubaini muundo wa silabi uliofikia upeo wa ukubalifu unabainishwa katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 7: Muundo wa Silabi wa Nazali, Konsonanti, Kiyeyusho na Irabu (NKYI)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		NKYI	H-KODA	FIKI-UKO
nkwi	a. \$nkwi\$i\$	**!	**	**
	b. \$n\$kwi\$	**!		**
	c. \$nkwi\$			

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Katika Jedwali Na. 7, umboshindani (a) linaonekana kuvunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Kadhalika, umboshindani (b) limevunja shartizuizi lenye nguvu na la mwisho kimpangilio. Aidha, umboshindani (c) halikuvunja shartizuizi lolote baina ya mashartizuizi kama yalivyo kimpangilio na hivyo kufikia upeo wa ukubalifu.

3.2 Muundo wa Silabi Nzito katika Kichasu

Kama tulivyobainisha katika kipengele kinachohusiana na dhana ya silabi nzito, kinachotazamwa katika miundo hii ni aina ya irabu inayounda silabi husika. Hii

ina maana kwamba irabu inayounda silabi nzito lazima iwe ndefu. Data Na. (8) huonesha utokeaji wa aina hii ya muundo.

(8)	mwire	\$mwi\$re\$	‘mwambie’
	kiyoo	\$ki\$yo:\$	‘kioo’
	ii	\$i:\$	‘hii’
	kuugwa	\$ku:\$gwa\$	‘kuanguka’
	kukaasi	\$ku\$ka:\$si\$	‘kukaa chini’

Chanzo: Kagaya (1989)

Data Na. (8), kwenye zile zenye hati iliyokoza, inaonesha kwamba katika Kichasu kuwapo kwa silabi nzito kunaweza kuwa matokeo ya michakato ya kifonolojia au ujibainishaji wa asili. Vilevile, silabi nzito huweza kujibainisha mwanzoni, kati au mwishoni mwa neno. Miundo ya silabi nzito katika Kichasu inawasilishwa katika vipengele vinavyofuata.

3.2.1 Muundo wa Irabu Ndefu (I:)

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, huu ni muundo unaojitokeza katika silabi za lugha ya Kichasu. Baadhi ya miundo ya aina hii ni matokeo ya michakato ya kifonolojia na mingine ni ya asili. Katika aina hii ya muundo, neno zima linaweza kuwa muundo kamili wa silabi. Tuchunguze Data Na. (9).

(9)	iiti	\$i:\$ti\$	‘kwamba’
	eendiwa	\$e:\$ndi\$wa\$	‘anatakiwa’
	uu	\$u:\$	‘huyu’

Chanzo: Kagaya (1989)

Jambo linalojibainisha katika Data Na. (9), hususani zile zilizoandikwa kwa hati iliyokoza, ni kwamba katika Kichasu muundo wa namna hiyo ni matokeo ya asili katika utamkaji wa silabi hizo. Vilevile, ujitekezaji wake unaweza kuwa mwanzoni au mwishoni mwa neno. Shartizuizi linalodhibiti aina hiyo ya muundo ni irabu ndefu, yaani I: linalohitajia kuwapo na mfuatano wa irabu mbili katika silabi. Mashartizuizi yanayotawala muundo huu yamepangiliwa kimfuatano kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

Jedwali Na. 8: Muundo wa Silabi wa Irabu Ndefu (I:)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		I:	FIKI-UKO	SHABI
iiti	a. \$i:\$ti\$			
	b. \$i\$i:\$ti\$	**!	**	*
	c. \$i\$iti\$	**!	**	*

Chanzo: Kagaya (1989)

Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8, umboshindani (a) linaonekana kufikia upeo wa ukubalifu kwani halijavunja shartizuizi lolote. Aidha, maumboshindani (b) na (c) yamevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Hivyo, yameshindwa kufikia upeo wa ukubalifu kulingana na sarufi ya lugha ya Kichasu.

3.2.2 Muundo wa Konsonanti na Irabu Ndefu (KI:)

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa lugha ya Kichasu inaruhusu mfuatano wa konsonanti na irabu ndefu katika silabi zake. Aina hii ya muundo huweza kujibainisha katika neno zima. Vilevile, kutokana na data za utafiti zilizokusanywa tumegundua kuwa ujitokezaji wake katika Kichasu huweza kuwa mwanzoni, kati au mwishoni kama inavyodhihirishwa na Data Na. (10).

(10)	mavee yoo kukaasi kubaa	\$ma\$ve:\$ \$yo:\$ \$ku\$ka:\$si\$ \$ku\$ba:\$	'maziwa' 'leo' 'kukaa chini' 'kuvunja'
------	----------------------------------	--	---

Chanzo: Kagaya (1989)

Jambo linalodhihirika katika Data Na. (10), hususani zile zenyе hati iliyokoza, ni kwamba aina hii ya muundo wa silabi hutokana na mchakato asilia wa kimatamshi miongoni mwa Wachasu wenyewe. Baada ya kuchunguza data nzima tuligundua kuwa hakuna mchakato wowote wa kifonolojia unaosababisha kutokea kwa irabu hizo ndefu. Vilevile, muundo wa aina hiyo unajitokeza zaidi mwanzoni mwa vitenzi ambapo wakati mwingine huhamia katika silabi ya pili katika mazingira ya kitenzi kuambikwa kiambishi awali. Shartizuizi linalodhibiti aina hiyo ya muundo ni lile linalohitajia kuwe na mfuatano wa konsonanti na irabu ndefu, yaani KI:. Mashartizuizi yanayotawala muundo huu yamepangiliwa kimfuatano katika Jedwali Na. 9.

Jedwali Na. 9: Muundo wa Silabi wa Konsonanti na Irabu Ndefu (KI:)

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		KI:	FIKI-UKO	SHABI
a. \$ku\$ba\$	**!	**	*	
b. \$kub\$a:\$	**!	**	*	
c. \$ku\$ba:\$				

Chanzo: Kagaya (1989)

Jambo linalojidhihirsha katika Jedwali Na. 9 ni kwamba maumboshindani (a) na (b), yenyewe yamevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Kwa upande wa umboshindani (c), lenyewe limefikia upeo wa ukubalifu kwani halikuvunja shartizuizi lolote. Hivyo, kufanya umbo hilo lifikie upeo wa ukubalifu katika Kichasu.

3.2.3 Muundo wa Nazali, Konsonanti na Irabu (NKI):

Kulingana na data za utafiti huu, Kichasu ni lugha ambayo inaruhusu mfuatano wa konsonanti mbili mfululizo zikifuaatiwa na irabu ndefu ambapo konsonanti ya kwanza ni nazali. Baada ya uchanganuzi wa data tuligundua kuwa ujibainishaji wa aina hii ya muundo huweza kuwa katika neno zima au sehemu ya neno kama inavyodhihirishwa na Data Na. (11).

(11) ngoo	\$ngo:\$	‘tumbili’
mpee	\$mpe:\$	‘sungura’
nkandeeni	\$nka\$nde:\$ni\$	‘pembezoni mwa ukuta’
kuangaa	\$ku\$a\$nga:\$	‘kupambazuka’

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Katika data Na. (11), kwenye zile zilizowekewa koza, tunaona namna ambavyo utamkaji asilia wa Wachasu umesababisha kuwapo kwa muundo huo wa silabi nzito. Kadhalika, shartizuizi lenye nguvu katika muundo huu wa silabi ni lile linalohitajia kuwapo kwa mfuatano wa nazali, konsonanti na irabu ndefu katika silabi, yaani NKI:. Mashartizuizi yanayotawala muundo huu yamepangiliwa kimfuatano katika Jedwali Na. 10 ili kusaidia kubainisha umbo lililofikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu.

Jedwali Na. 10: Muundo wa Silabi wa Nazali, Konsonanti na Irabu (NKI):

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI		
		NKI:	FIKI-UKO	SHABI
mpee	a. \$m\$pe:\$	**!	**	*
	b. \$mpe\$	**!	**	*
	c. \$mpe:\$			

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Data katika Jedwali Na. 10 inaonesha kwamba maumboshindani (a) na (b) yamevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili na la mwisho kimpangilio. Kinyume na hilo, umboshindani (c) limeweza kushinda dhidi ya maumbo yaliyoshindanishwa kwani halikuvunja shartizuizi lolote katika Kichasu na hivyo kufikia upeo wa ukubalifu.

3.2.4 Muundo wa Nazali, Kiyeyusho na Irabu (NYI):

Silabi za Kichasu, kulingana na data zilizokusanya, zinaruhusu mfuatano wa nazali, kiyeyusho na irabu ndefu. Katika data tulizozikusanya uwandani na baada ya kuchanganua data nzima tulibaini kuwa aina hii ya muundo haijibainishi sana katika Kichasu. Data Na. (12) inadhihirisha ujitekezaji huo.

(12) nywii	\$jwi:\$	‘nywele’
mweza	\$mwe:\$za\$	‘mrefu’

mwire \$mwi:\$re\$ ‘mwambie’
Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Data Na. (12), katika zile zilizowekewa hati iliyokoza, inaonesha kwamba baadhi ya miundo imetokana na urefushaji wa irabu asilia, kwa mfano, \$jwi:\$, na mingine imetokana na michakato mingine ya kifonolojia ikiwamo uyeyushaji kama vile katika maneno \$mwe:\$nza\$ na \$mwi:\$re\$. Shartizuizi linalodhibiti aina hiyo ya muundo ni lile linalohitajia kuwapo kwa mfuatano wa nazali, kiyeyusho na irabu ndefu katika silabi, yaani NYI:. Mashartizuizi yamepangwa kimfuatano katika Jedwali Na. 11, ili kubaini muundo ulioweza kufikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu kwa kutokuvunja shartizuizi lolote.

Jedwali Na. 11: Muundo wa Silabi wa Nazali, Kiyeyusho na Irabu (NYI):

INGIZO	MAUMBOSHINDANI	MASHARTIZUIZI			
		NYI:	H-KODA	FIKI-UKO	SHABI
mwire	a. \$mwi:\$re\$				
	b. \$mwi:\$re\$	**!		**	*
	c. \$mwi:\$re\$	**!	**	**	*

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Katika Jedwali Na. 11 tunaona kuwa umboshindani (a) limekuwa mshindi kati ya maumbo yote yaliyoshindanishwa kwani halikuvunja shartizuizi lolote kama yalivyo katika mpangilio. Kwa minajili hiyo, umboshindani (b) limevunja shartizuizi lenye nguvu, la tatu na la mwisho kimpangilio. Umboshindani (c) limevunja shartizuizi lenye nguvu, la pili, la tatu na la mwisho kimpangilio. Hivyo, maumboshindani hayo yameshindwa kufikia upeo wa ukubalifu katika Kichasu.

Baada ya kuona uchanganuzi wa muundo wa silabi za Kichasu kwa kuzingatia mashartizuizi ya Kichasu, imedhihirika kuwa lugha ya Kichasu inaangukia katika muundo msingi wa KI. Hivyo, silabi zake huundwa na sehemu kuu mbili ambazo ni mwanzosilabi na kilele cha silabi. Hivyo, kwa maneno mengine Kichasu kina muundo wa silabi huru. Ni vyema tukaweka wazi kwamba baadhi ya miundo ya silabi za lugha ya Kichasu haina mwanzosilabi, hasa ile inayoundwa na irabu. Kwa kuwa ujitokezaji wa miundo hiyo hutegemea kanuni na taratibu zinazoongoza upangiliaji wa fonimu ili kupata muundo kamilifu wa silabi, uchanganuzi wa muundo wa silabi za lugha ya Kichasu ulizingatia mashartizuizi ya lugha hiyo katika kuunda silabi zake.

4.0 Hitimisho

Utafiti huu umebaini kuwa Kichasu kina jumla ya miundo kumi na mmoja (11) ya silabi ambayo inakubalika. Miundo hiyo ni ya silabi nyepesi ambayo ni: irabu pekee (I); konsonanti na irabu (KI); nazali pekee (N); nazali, konsonanti na irabu (NKI); nazali, kiyeyusho na irabu (NYI); konsonanti, kiyeyusho na irabu (KYI) pamoja na nazali, konsonanti, kiyeyusho na irabu (NKYI). Katika silabi nzito ni

irabu ndefu pekee (I:); konsonanti na irabu ndefu (KI:); nazali, konsonanti na irabu ndefu (NKI:) pamoja na nazali, kiyeyusho na irabu ndefu (NYI:). Baadhi ya miundo tulioibainisha inajitokeza pia katika lugha zingine za Kibantu, ijapokuwa miundo fulanifulani hajitokezi katika lugha zingine. Katika hatua nyingine, utafiti umebaini kuwa Kichasu, kama lugha nyinginezo za Kibantu, kina muundo msingi wa KI wenyе shartizuizi la msingi linaloongoza miundo mingi ambapo linahitaji kila muundo wa silabi uishie na irabu. Ujitokezaji wa muundo msingi wa silabi unaweza kuwa mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. Kwa hivyo, utafiti huu umechangana kwa kina muundo wa silabi za Kichasu na ambao una mchango muhimu katika matumizi ya Nadharia ya Umbo Upeo kwa kuchanganua kipengele cha silabi kwa kuzingatia mashartizuizi.

Marejeleo

- Abercrombie, D. (1967). *Elements of General Phonetics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Charles, A. (2011). Fonolojia ya Kigweno: Miundo ya Silabi na Michakato ya Kifonolojia. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Choti, N.J. (2015). Phonological (A)symmetries of Nasal Prefixes in Bantu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Michigan.
- Clark, J. na Yallop, C. (1990). *An Introduction to Phonetics and Phonology*. Oxford: Blackwell.
- Clements, G. na Keyser, J.S. (1983). *Cv Phonology: A Generative Theory of the Syllable*. Cambridge: The MIT Press.
- Downing, L.J. na Mtenje, A. (2017). *The Phonology of Chichewa*. Oxford: Oxford University Press.
- Etakwa, E. (2019). The Phonology of Olutura Syllable. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Fery, C. na Vijver, R. (2003). *The Syllable in Optimality Theory*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hyman, L.M. (1985). *A Theory of Phonological Weight*. Dordrecht: Foris Publications.
- Hyman, L.M. (2003). "Basaa (A43)." Katika D. Nurse na G. Philippson (Wah.), *The Bantu Language*. London: Routledge. Kur. 257-282.
- Hyman, L.M. na Katamba, F. (1999). "The Syllable in Luganda Phonology and Morphology." Katika, H. Hulst na N. Ritter (Wah.), *The Syllable: Views and Facts*. Berlin: Mouton de Gruyter. Kur. 349-416.
- Judica, E. (2014). Muundo wa Silabi katika Kimashami. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Juma, M. (2018). The Sociolinguistic, Semantic and Morphological Characteristics of Personal Names in Southern Chasu. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Kagaya, R. (1989). *A Classified Vocabulary of the Pare Language*. Tokyo: Institute for the Study of Languages and Cultures of Asia and Africa.
- Kager, R. (2004). *Optimality Theory*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Katamba, F. (1989). *An Introduction to Phonology*. London: Longman.
- Kenstowicz, M. (1994). *Phonology in Generative Grammar*. Cambridge: Oxford University Press.
- Kigume, R.A. (2010). The Syllable Structure in Kingindo: The Case of Kimagingo Variety. *Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kimizi, M.M. (2003). The Syllable Structure in Standard Kiswahili. *Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Kindija, K.A. (2003). Syllable Presentation in Kisukuma: The Case of Jidakama Dialect. *Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kotz, E. (1909). *Grammatik des Chasu in Deutsch-Ostafrika*. Berlin: The Gregg Press.
- Ladefoged, P.L. (2000). *A Course in Phonetics* (Tol. 4). Canberra: Thomas Wordsworth.
- LOT. (2009). *Atlas of the Languages of Tanzania*. Dar es salaam: LOT.
- Maho, J.F. (2009). A Referential Classification of the Bantu Languages. Inapatikana katika https://brill.com/fileasset/downloads_products/35125_Bantu-New-updated-Guthrie-List.pdf. Ilisomwa tarehe 23 Oktoba 2022
- Mreta, Y.A. (1998). *An Analysis of Tense and Aspects in Chasu: Their Form and Meaning in the Affirmative Constructions*. Hamburg-German: LIT Verlag.
- Mreta, Y.A. (2008). *Chasu: Kamusi ya Chasu - Kiingereza - Kiswahili (Chasu-English-Swahili Dictionary)*. Dar es Salaam: LOT.
- Massamba, D.P.B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nkamigbo, L.C. (2015). "A Constraint-Based Account of Koring Syllable Structure." *Unizik Journal of Arts and Humanities*. 16(2): 1-18.
- Nurse, D. na Philippson, G. (2003). *Towards a Historical Classification of the Bantu Language*. New York: Taylor & Francis Routledge.
- Odden, D. (2006). "Minimality and Onsetless Syllable in Zinza." *Phonology*. 23(3): 43-441.
- Odden, D. (2015). "Bantu Phonology." *Working Paper in Linguistic*. 60: 102-110.
- Odden, D. na Odden, M. (1999). "Kihehe Syllable Structure." Katika H. Hulst na N. Ritter (Wah.), *The Syllable: Views and Facts*. Berlin: Mourton de Gruyter. Kur. 417-445.
- Omari, C.K. (1991). God and Worship in Traditional Asu Society. Erlangen: Verlag der Ev.-Luth Mission.

- Persohn, B. (2017). *The Verb in Nyakyusa: A Focus on Tense, Aspect and Modality*. Berlin: Language Science Press.
- Prince, A. na Smolensky, P. (1993). *Optimality Theory: Constraints Interactions in Generative Grammar*. New Brunswick: Rutgers University.
- Vaux, B. na Cooper, J. (2003). *Introduction to Linguistic Field Methods*. Muenchen: LINCOM EUROPA.
- Yohana, R. (2009). A Sociolinguistic Analysis of Variation in a Rural African Community. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Cape Town.
- Zacharia, S.B. (2013). A Study of Syllable Structure in Kiha: A Case Study of Kasulu-Kiha Variety. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino cha Tanzania.